

Safari Ambayo Sitaisahau Maishani Mwangu

Ninaipenda familia yangu sana. Tunapenda kusafiri pamoja kila kiangazi. Mimi na familia yangu tunasafiri pwani magharibi mwa Marekani katika jimbo la Oregon. Si safari ninayofurahia sana zaidi, lakini ninapenda pwani sana. Kabla ya kusimulia safari yetu, ninataka kufafanua familia yangu.

Familia yangu ina watu watano: mimi, kaka yangu, dada yangu, na mama na baba. Tunatoka mji wa Seattle, jimbo la Washington. Seattle ni mji mzuri sana kwa sababu kuna miti mingi sana na milima mikubwa. Ingawa Seattle ni nzuri, kuna mvua sana! Niliishi katika Seattle na familia yangu kwa muda wa miaka kumi na nane halafu tukahamia California kusini karibu na mji wa Los Angeles. Tulihamia Los Angeles kwa sababu mama alipata kazi bora zaidi. Tumeishi karibu na Los Angeles kwa muda wa miaka miwili. Tunapenda California sana kwa sababu hali ya hewa ni nzuri sana na hakuna mvua nyingi.

Sasa, kaka yangu anaishi nyumbani pamoja na wazazi wangu kwa sababu yeye ni mwanafunzi wa shule ya sekondari. Anasoma bayolojia, fizikia na fasihi. Ingawa yeye ni mwanamichezo na huogelea kila siku, anapata alama nzuri masomoni. Kwa hivyo, mwaka ujao atajiunga na Chuo Kikuu cha Yale.

Mimi na dada yangu hatuishi nyumbani. Ninakaa Stanford kwa sababu mimi ni mwanafunzi wa chuo kikuu. Ninaishi bwani la Columbae. Ninasoma bayolojia, kemia na Kiswahili. Nitapata shahada yangu ya kwanza ya bayolojia mwaka ujao. Dada yangu anaitwa Carole na anaishi San Francisco kwa sababu anafanya kazi huko. Ameishi San Francisco kwa muda wa miezi kumi. Alisoma katika Chuo Kikuu cha Stanford kama mimi lakini alipata shahada yake ya kwanza ya isimu ya lugha.

Mama yangu anaitwa Cathy. Ana dada wawili. Mmoja anaitwa Carol, kama dada yangu, na Libby. Mama yangu anafanana na dada yake. Wanatutembelea katika nyumba yetu sana kwa sababu wanapenda kusafiri. Mama yangu ni mtakwimu na anafanya kazi kwenye

Alaina Critchlow
Beginning Swahili 106B
Writing Assignment

kampuni ya Amgen. Amgen hushughulika na bayolojia na kemia. Katika nyumba, mama yangu anapenda kupika. Baba yangu anaitwa Steve na anafanya kazi kwenye kampuni ya Akademia 123 karibu na Los Angeles. Akademia 123 hushughulika na hesabu. Mama na baba yangu walisomea Chuo Kikuu cha Stanford kama dada yangu na mimi. Familia yote inapenda kusoma na kujifunza.

Ingawa tunapenda kusoma, tunapenda kusafiri pia. Kila kiangazi tunazuru kijiji cha Manzanita katika pwani ya jimbo la Oregon. Katika Manzanita kuna watu wachache kwa hivyo tunaweza kupumzika na kubarizi. Wakati wa kusafiri Manzanita, tunaenda kwa motokaa. Aghalabu, tunaamka mapema na tunafunga mizigo. Baada ya kufunga mizigo tunaendesha motokaa mpaka tunafika Manzanita. Ni safari ya muda wa masaa matano bila kusimama njiani. Tunaondoka baada ya kula chakula cha asubuhi na tunafika kabla ya chakula cha mchana. Baba yangu ni dereva wa motokaa na anaendesha upesi lakini ni sawasawa kwa sababu anaendesha vizuri.

Tunakaa Manzanita kwa muda wa wiki moja. Tunaenda kutembelea kijiji kingine kwa muda wa siku moja ili kujifunza kuhusu kijiji kile. Hutembelea vijiji vya Tillamook, Cannon Beach, Astoria na vijiji vingi vingine. Safari niliyofurahia zaidi ni ya Tillamook kwa sababu watu hutengeneza maziwa na jibini huko. Ninapenda Manzanita zaidi kwa sababu katika Manzanita tunaogelea baharini na tunatembea pwani. Tunaona ndege na samaki. Usiku tunaona nyota nyingi. Pia tunaendesha baisikeli na tunacheza gofu, tenisi na michezo mingine. Wakati wa kukaa Manzanita, ninapenda kupumzika na kusoma vitabu vingi. Ninasoma mada nyingi, kama mapenzi na historia. Ninafurahi sana katika Manzanita.

Sitarudi Manzanita kiangazi hiki kwa sababu nitahitaji kufanya kazi na kusoma. Ningetaka kurudi Manzanita hivi karibuni ili kupumzika na kuwa na familia yangu. Tunapenda kukaa Manzanita na tunataka kununua nyumba huko.